

UHFUNDI KATIKA MILKI

1. ROHO

NYENZO

- Utepe uliojikunjakunja, sentimita 50
- Roho ya karatasi
- Bango lililo na Mstari wa Biblia
- Gundu
- Rangi

MAELEKEZO

1. Kata roho na bendera. Zipake rangi kwa kutumia rangi unazozipenda zaidi.
2. Kwa kutumia gundi shikanisha peo zote mbili za utepe hadi nyuma ya roho ili kuunda kitanzi. Kwa kutumia gundi shikanisha kipande cha bendera sehemu ya katikati utepe.



2. TANURI

NYENZO

- Utako wa Karatasi ya tanuri
- Maumbo ya moto wa Karatasi
- Rangi
- Gundu

MAELEKEZO

1. Kata tanuri na moto. Paka rangi katikati ya tanuri na moto na watu (kumbuka kuwa watu hawa hawakuumia).
2. Paka rangi moto na rangi ya machungwa, manjano, na nyekundu ili kufanana na moto.
3. Kunja kingo za pande za moto na uzitie gundi na kuzibandika katika tanuri ili zifunguke kama moto.




3. KOFIA YA KIBABELI

NYENZO

- Kiolezo cha Karatasi
- Rangi
- Gundu
- Utepe uliojikunjakunja, 50 sentimita

MAELEKEZO

1. Kata kiolezo cha kofia. Paka rangi.
2. Kunja katika mistari ilio na nukta na kuifanya kofia kujilalia kidogo kana kwamba ni vipande 3 tofauti.
3. Shikanisha utepe uliojikunjakunja katika mashimo yaliyo katika kila upande na kuifunga kichwani.
4. Irembeshe na vimetameta.





4. FREMU YA PICHA

NYENZO

- Kiolezo cha fremu kutoka kwa karatasi iliyo na upovu au rangi
- Taji 3 za karatasi
- Herufi "Mimi ni jasiri"
- $\frac{1}{2}$ mrija wa kunywea
- Utepe uliojikunjakunja
- Gundi



MAELEKEZO

1. Kata kiolezo cha fremu na kuondoa vipande veya ziada.
2. Ikuje nusu na kutia gundi na kushikanisha kingo 3 katika ya 4. Wacha kingo ya 4 ikiwa imefunguka na kutia picha na kuacha kanda zilizo juu kama zimefunguka ili kutia mrija wa kunywea.
3. Unaweza kuchapisha picha au kuwaambia watoto wachore picha ya Esta na kuitia katika fremu.
4. Rembesha taji na barua "Mimi ni jasiri."
5. Kumalizia, tia mrija wa kunywea katika kanda zilizoko juu na kufunga utepe uliojikunjakunja katika pande zote mbili za mrija na kuning'iniza fremu ya picha.

5. BARAKOA YA SIMBA

NYENZO

- Shina la barakoa
- Karatasi ya povu ya manjano au karatasi ya rangi iliyo na uso
- Karatasi ya povu ya rangi ya machungwa au karatasi ya rangi ya maskio, nyusi, na pua
- Karatasi ya povu nyeupe au karatasi ya mdomo
- Utepe uliojikunjakunja, 50 sentimita
- Rangi
- Gundi



MAELEKEZO

1. Kata shina la barakoa na kulipaka rangi.
2. Weka gundi na kushikanisha povu/karatasi ya manjano hapo juu kama ilivyoonyeshwa katika picha iliyopo hapa.
3. Juu ya hilo, weka gundi katika kinywa na kisha katika pua hapo juu. Pia weka gundi katika masikio na kovu kama ilivyoonyeshwa katika picha.
4. Funga utepe uliojikunjakunja katika mashimo katika pembe zote mbili ili itoshee katika kichwa cha mtoto.

